**HOTUBA YA MGENI RASMI, MHE RABIA HUSSEIN KATIKA KUADHIMISHA SIKU YA ADHABU YA KIFO DUNIANI ILIYOTOLEWA TAREHE 10 OKTOBA, 2013 KATIKA UKUMBI WA KITUO CHA HUDUMA ZA SHERIA ZANZIBAR**

Ndg. Mwenyekiti wa mkutano huu,

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Kituo Cha Huduma za Sheria Zanzibar, Profesa Chris Maina Peter

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar na watendaji wako waliohudhuria,

Viongozi wa Taasisi mbali mbali za Serikali na za Kiraia mliohudhuria,

Viongozi wa dini mliohudhuria,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Asaalam Aleykum,

Awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kutuwezesha kwa pamoja kufika hapa tukiwa wenye afya njema. Kwa uwezo wake tukaweza kuitana hapa na kujumuika kwa pamoja katika kuungana na wenzetu kwa kuadhimisha siku hii.

Pili napenda kuchukua fursa hii adhimu kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) ambao ni waandaaji na wasimamizi wa maadhimisho haya kwa heshima mlionipa ya kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika kuadhimisha siku ya adhabu ya kifo duniani.

Ndugu Mwenyekiti,

Hii ni mara yangu ya kwanza kualikwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar kuwa mgeni rasmi. Kwa upande wangu najihisi nami ni mmoja wa watoa huduma za sheria kwa jamii kama kazi zenu za kila siku zinavyowataka. Sina maneno makubwa zaidi ya kusema kuwa nathamini sana heshima hii mliyonipa na kuahidi kuitunza.

Ndugu Mwenyekiti,

Inafahamika kuwa ifikapo tarehe hii ya leo, tarehe 10 Mwezi wa Oktoba, nchi zilizo wanachama wa umoja wa mataifa zinaadhimisha siku ya adhabu ya kifo duniani. Umoja wa Mataifa imeteua siku hii kila mwaka kupinga adhabu ya Kifo duniani kote.

Nchi nyingi zilizo ridhia mkataba wa Umoja wa Mataifa zinafanya juhudi za makusudi za kupinga adhabu ya kifo kwa watuhumiwa wa makosa mbalimbali. Kwa takwimu za hivi karibuni, hadi kufikia mwaka huu nchi 58 tu ndizo zilizofuta adhabu hiyo ya kifo ambapo kwa Afrika ni nchi chache sana kati ya hizo 58.

Uadhimishaji huu hufanyika kwa shughuli mbalimbali zikiwemo kuandaa semina, warsha au makongamano kwa madhumuni ya kutoa ujumbe wa kupinga adhabu ya kifo. Nimefarijika sana kuona Kituo kimelazimika kuadhimisha siku hii ya adhabu ya kifo duniani.

Ndugu mwenyekiti,

Kwa miaka mingi sasa adhabu ya kifo katika nchi yetu na duniani, inachukuliwa kama ni moja ya adhabu halali kama zilivyo adhabu nyengine zinazopaswa kutolewa kwa yeyote aliepatikana na hatia ya kufanya kosa la jinai. Kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Jinai Namba 6 ya mwaka 2004 Sheria za Zanzibar na hata kwa Sheria ya Makosa ya Jinai Ya Tanzania Bara kosa la mauaji ya kukusudia na uhaini ni makosa ambayo kwa anaepatikana na hatia basi adhabu yake ni kifo.

Kasi ya kuondoa kabisa adhabu ya kifo sio kubwa sana na mjadala wake umegawika katika makundi mawili. Kuna wale wanaounga mkono adhabu hii iendelee na kuna wale wanaotaka adhabu hii isiendelee. Wale wanaotaka adhabu ya kifo iendelee wanaamini kwamba kutekelezwa kwake ni muhimu kwa vile inahakikisha kutendeka kwa haki kwa yule aliyeondolewa uhai wake kwa nia ovu na makusudi na pia kwa familia yake. Pia kundi hili linaona kuwa adhabu ya kifo ni adhabu sahihi kwa vile kuua kwa makusudi ni kosa kubwa sana ambapo kama adhabu kali itatolewa itapelekea watu wengine watakaoona au kusikia utekelezaji wa adhabu hii kuogopa na kutofanya kosa la aina hiyo.

Kundi la pili ni lile linaloona adhabu hii ya kifo ni adhabu katili sana, si ya kibinaadamu, inadhalilisha na haifai kukubalika kama adhabu. Kundi hili linaona kuwa adhabu ya kifo inakwenda kinyume na haki za kibinaadam na ikishatekelezwa basi haiwezi kutenguliwa.

Kwa Tanzania utaratibu huu wa kutekeleza adhabu ya kifo bado upo kwenye mjadala na jamii pamoja na Taasisi mbalimbali ambazo zinajaribu kutoa maoni yao na kupendekeza kuondolewa kwa aina hizi za adhabu. Wanaharakati wamekua katika mstari wa mbele kushajihisha kuhamasisha umma pamoja na serikali kufikiria kuondoa adhabu ya kifo.

Ukweli ni kwamba adhabu ya kifo ni adhabu inayochukua uhai wa binaadamu hata kama imetolewa na Sheria. Pia mtendaji wa kosa kama la kuua kwa makusudi huwa amechukuwa uhai wa binadamu mwengine, uhai ambao hakupaswa kuuchukuwa na uhai ambao unalindwa na Katiba zetu pamoja na dini zetu.

Kuthaminiwa kwa uhai wa mtu ndio sababu kuu iliyopelekea kuwepo kwa wazo la kuiondoa adhabu hii katika orodha za adhabu za makosa. Lengo likiwa ni kujaribu kutoa heshima ya uhai kwa kila mwanaadamu. Dhana ya adhabu inabaki palepale katika lengo la kuzuia makosa yasitendeke zaidi. Na ndio maana ujumbe wa mwaka huu wa kuadhimishi siku hii ya leo ukasema **"stop the crime and not life" yaani zuia uhalifu na sio uhai.**

Ndugu mwenyekiti,

Kama nilivyosema awali hapa kwetu Tanzania bado tunavyo vifungu vya sheria vinavyotoa adhabu ya kifo katika Sheria za uhalifu. Na kwa kufuata vifungu hivyo, Mahakama Kuu zimepewa mamlaka ya kuamuru mtu yeyote alietiwa hatiani na vifungu hivyo kuadhibiwa kifo.

Ndugu mwenyekiti,

Ninafahamu kwamba katika miaka ya hivi karibuni, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia tume ya kurekebisha Sheria (Law Reform Commission) ilifanya utafiti juu ya adhabu ya kifo na kutoa mapendekezo yake Serikalini. Mbali na juhudi hizi za ndani, Mkataba wa Ziada (Protocol) wa kimataifa wa mwaka1987 na mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966 (International Covenant on Civil and Political Rights of 1966) unazitaka nchi ambazo zimeweka saini na kuuridhia, kuanzisha utaratibu wa kuindosha adhabu hii katika vitabu vyake vya sheria. Kwa bahati mbaya Tanzania bado haijaridhia Mkataba huu wa ziada wa mwaka 1987.

Ndugu mwenyekiti,

Ninafahamu pia kuna wanazuoni wanaharakati wa haki Za Binaadamu wametunga vitabu mbali mbali kuhusu Adhabu ya kifo, moja ya kitabu hicho kinaitwa *Adhabu ya Kifo katika Sheria za Kiislamu*, kilichotungwa na mwanazuoni maarufu hapa Zanzibar Dr. Muhyiddin Ahmad Khamis *Maalim Siasa* . Kitabu hichi kinaelezea nidhamu ya kifo katika uislamu ni nyenzo katika nyenzo ambazo zinategemewa katika kuhifadhi jamii kuepukana na uovu wa kupita mipaka.

Hata hivyo waumini wa dini ya Kiislamu wanahoji utaratibu unaofuatwa katika kutoa adhabu ya kifo kama unafanana na utaratibu uliolezwa katika Kitabu Kitukufu cha Quran.

Kwa upande wa dini nyengine kwa mfano dini ya kikristo, katika Agano la Kale ipo Adhabu ya kifo. Lakini katika Agano Jipya Adhabu hio imeondolewa.

Ndugu Mwenyekiti,

Nchi yetu bado haijaridhia tamko la Kimataifa kuhusu kupinga adhabu ya kifo. Kwa sasa, kwa kuwa sheria hii ya kifo bado haijafutwa ni vyema wananchi kuendelea kuijadili faida na hasara zake mpaka pale Serikali itakapopima na kuona kama ipo haja ya kuiondosha adhabu hii.

Mwisho,

Waheshimiwa mliohudhuria, sasa nachukua nafasi hii kutamka kwamba  mjadala huu wa adhabu ya kifo uliyoandaliwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar umefunguliwa rasmi.

**Ahsanteni sana kwa kinisikiliza.**